

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA NNE

05 NOVEMBA, 2021



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA NNE – TAREHE 05 NOVEMBA, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**39. MHESHIMIWA MRISHO MASHAKA GAMBO  
(ARUSHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wanapata malipo kama Madiwani na Wabunge kutokana na majukumu mazito wanayoyafanya ikiwemo ufuatiliaji wa malipo ya Kodi ya Majengo.

**40. MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA (BUYUNGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Zahanati na Vituo vya Afya katika Wilaya ya Kakonko.

**41. MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGINDU BUTONDO (KISHAPU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro uliopo mpakani mwa Wilaya ya Kishapu Kata ya Mwamalasa Kijiji cha Magalata na Wilaya ya Iramba.

**WIZARA YA MAJI:**

**42. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini tatizo la maji litakwisha katika Mji Mdogo wa Mikumi.

### **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

#### **43. MHESHIMIWA DKT. STEVEN LEMOMO KIRUSWA (LONGIDO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi:-

Je, ni lini Serikali itaboresha miundombinu ya Minada ya Mifugo kwa kujenga mazizi ya kisasa, vyoo na ofisi za kupokea tozo na kodi za mnada.

### **WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

#### **44. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini Serikali italifuta Shamba la Mwakinyumbi Estate lililotolekezwa kwa muda mrefu na kuwapa Wananchi wa Hale na maeneo jirani ili waweze kufanya shughuli za kiuchumi.

## **WIZARA YA MADINI:**

### **45. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro uliopo katika eneo lenye Madini ya Jasi kati ya Wananchi wa Kata ya Bendera Mkoani Kilimanjaro na Wananchi wa Kata ya Mkomazi Mkoani Tanga.



## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **46. MHESHIMIWA AMSABI JEREMIAH MRIMI (SERENGETI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza Viwanja vya Ndege ndani ya Hifadhi ya Serengeti kwa kujenga Uwanja wa Ndege katika Mji wa Mugumu nje kidogo ya Hifadhi pamoja na kukamilisha ujenzi wa barabara ya lami ya Makutano Sanzate Natta na ile ya Tarime Mugumu Natta.

## **WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

### **47. MHESHIMIWA HASSAN SELEMAN MTENGA (MTWARA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni lini Serikali itashughulikia urejeshwaji wa fedha za Wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini ambao walijiunga na *Pride* kwa ajili ya kupata mikopo.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **48. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itatoa GN kuwezesha Mradi wa *Regrow* kuanza rasmi katika eneo la Kihesa.

### **III. KAMATI YA MIPANGO:**

#### **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge lipokee, Kujadili na Kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka 2022/2023 pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.



*(Majadiliano yanaendelea)*

DODOMA  
05 NOVEMBA, 2021

N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE